# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 050 FEBRUARI 2025

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY




## 1 TMA NA EMEDO WAONGEZA NGUVU USAMBAZAJI WA TAAARIFA ZA HALI YA HEWA ZIWA VICTORIA

## 2 DKT. CHANG'A AONGOZA MKUTANO WA 62 WA JOPO LA KIMATAIFA LA SAYANSI YA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI (IPCC-62)




## 3 FAHAMU ZAIDI:
## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI, 2025



## KITAIFA

# TMA NA EMEDO WAONGEZA NGUVU USAMBAZAJI WA TAARIFA ZA HALI YA HEWA ZIWA VIKTORIA

**Dodoma**



Katika kuendelea kuboresha usambazaji wa taarifa za hali ya hewa kwa jamii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilitembelewa na Wataalamu wa Shirika lisilo la Kiserikali la Uhifadhi wa Mazingira na Maendeleo ya Kiuchumi la EMEDO ambalo linalojihusisha na uhifadhi wa mazingira katika maeneo yanayozunguka Ziwa Viktoria. Ziara ya EMEDO ilikuwa na lengo la kujadiliana namna ya kuendelea kushirikiana katika usambazaji wa taarifaza hali ya hewa ili kuwafikia wananchi wengi zaidi wa maeneo yanayozunguka Ziwa Viktoria hususani wavuvi. Kikao kati ya TMA na EMEDO kilifanyika Februari 4, 2025 kwenye Ofisi za TMA Makao Makuu, Jijini Dodoma.


Wakati wa ziara hiyo yalifanyika majaribio ya matumizi ya kifaa maalumu cha usambazaji wa taarifa za hali ya hewa "Electronic Weather Board", ambacho kitawasaidia wavuvi na watumiaji wa Ziwa Viktoria kwenye kisiwa cha Goziba kuona utabiri wa hali ya hewa unaotarajiwa katika ziwa kwa lengo la kufanya maamuzi sahihi ili kuokoa maisha na mali.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA Dkt.Ladislaus Chang'a aliushukuru uongozi wa Shirika la EMEDO kwa ushirikiano unaoendelea kati ya taasisi hizi wenye lengo la kusambaza taarifa na

elimu ya matumizi sahihi ya taarifa zitolewazo na TMA katika maeneo ya ziwa Victoria.

“Haya ni mambo muhimu sana tunapaswa kufanya ili kuoanisha shughuli zetu na maono ya kimkakati na kuleta thamani kwa kile tunachofanya. Nimevutiwa sana na ushirikiano huu kwa sababu tunataka kila mmoja wetu kuchangia katika kufikia maono ya Taifa. Kwa mfano, kuimarisha hatua zakijamii kuhusu mabadiliko ya tabianchi na kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa Duniani”. Alisema Dkt. Chang’a.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa EMEDO, Bi. Editrudith Lukanga, aliishukuru pia Mamlaka kwa ushirikiano huu  na kusema kuwa TMA imekuwa ikitoa wataalamu wake katika kutoa mafunzo kwa jamii na pia kutoa utabiri wa hali ya hewa, jambo ambalo limekuwa na manufaa kwa  jamii.




Kwa upande wake Meneja Mradi wa EMEDO, Bw. Arthur Mugema alisisitiza kuwa ushirikiano kati ya taasisi hizi ndio umeleta matokeo ya kuandaa na kuweka kifaa cha  kielektroniki (Electronic Weather Board) kwenye kisiwa cha Goziba ambacho kinaenda kuboresha upatikanaji wa taarifa za hali ya  hewa.



## KIMATAIFA

# DKT. CHANG'A AONGOZA MKUTANO WA 62 WA JOPO LA KIMATAIFA LA SAYANSI YA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI (IPCC-62)

**Hangzhou, China**




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ambaye pia ni Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi "Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC)", Dkt. Ladislaus Chang'a, alishiriki kuongoza Mkutano wa 62 wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi *"The Sixty-Second Session of the Inter-Governmental Panel on Climate Change (IPCC 62)".*


Mkutano wa IPCC-62 ulifanyika Hangzhou, China kuanzia tarehe 24 hadi 28 Februari, 2025 ambapo lengo la mkutano huo lilikuwa ni kujadili na kupitisha miundo ya taarifa zinazotarajiwa kuandaliwa na Vikosikazi vinavyounda Jopo la IPCC (*Working Group I, Working Group II, Working Group III, na Task Force on National Greenhouse Gas Inventories -TFI).* Taarifa zitakazoandaliwa na Vikosikazi hivyo ndizo zitajumuishwa pamoja na kuandaa taarifa ya ujumla ya Mzunguko wa Saba wa Tathmini ya IPCC ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi "*IPCC Seventh Assessment*

*Cycle Report (AR7)"*. Mzunguko wa saba (7) wa Tathmini ya IPCC ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi ulianza mwaka 2023 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2029.

Katika Mkutano huo, Vikosikazi vya Jopo la IPCC viliwasilisha mapendekezo ya miundo ya taarifa zao katika mzunguko wa saba, ambapo wajumbe wa Jopo hilo walizijadili na kuzipitisha. Dkt. Chang'a ambaye ni miongoni mwa viongozi wa Jopo la IPCC kwa nafasi ya Makamu Mwenyekti alishiriki katika kuongoza vikao vilivyojadili na kupitisha mapendekezo yaliyowasilishwa.

Mkutano wa IPCC-62 ulihudhuriwa na viongozi wa IPCC, maafisa viungo wa nchi wanachama wa IPCC (IPCC Focal Points), wanasayansi ya hali ya hewa, washirika wa maendeleo na wadau mbalimbali walioalikwa katika mkutano huo. Washiriki kutoka Tanzania alikuwa ni Dkt. Chang'a ambaye aliambatana na Meneja Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa wa TMA katika masuala ya Hali ya Hewa, ambaye pia ni Afisa Kiungo wa Tanzania katika Jopo la IPCC (IPCC Focal Point for Tanzania), Bw. Wilbert Muruke.

Katika hatua nyingine, Dkt. Chang'a alikutana na Mkuu wa Taasisi ya Hali ya Hewa ya China (China Meteorological Administration -CMA) Dkt. Chen Zhenlin, ambapo viongozi hao walijadili maeneo ambayo TMA inaweza kushirikiana na CMA katika masuala ya hali ya hewa katika muktadha mzima wa kuboresha zaidi huduma za hali ya hewa katika nchi zetu mbili. Miongoni mwa maeneo ya ushirikiano waliyojadili ni matumizi ya teknolojia ya Akili Mnemba (Artificial Intelligence-AI) katika utabiri wa hali ya hewa, ambayo inaweza kuchangia kuongeza zaidi usahihi wa utabiri wa hali ya hewa unaotolewa na TMA kwa jamii.



## FAHAMU ZAIDI

### HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI, 2025

Katika kipindi cha mwezi Machi, 2025 mvua za Masika zinatarajiwa kuanza katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, ilhali mvua za Msimu zinatarajiwa kuendelea katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka.. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini na kusababisha mafuriko katika baadhi ya maeneo. Kwa upande mwingine, hali ya joto inatarajiwa kupungua kidogo, aidha katika baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kuwa na upungufu wa mvua hali ya joto inatarajiwa kuendelea.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| **Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):** | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya pili ya mwezi.** |
| **Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):** | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika wiki ya pili ya mwezi.** |
| **Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):** | ♦ Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya pili ya mwezi.** |
| **Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** | ♦ Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya pili.** |
| **Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya pili ya mwezi.** |
| **Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):** | ♦ Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa kati ya wiki ya kwanza na ya pili katika maeneo machache.** |
| **Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** | ♦ Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya pili ya mwezi.** |
| **Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma):** | ♦ Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |

## JE WAJUA?

Tarehe 23 machi kila mwaka, Tanzania kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) huungana na nchi nyingine wanachama wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) kuadhimisha Siku ya Hali ya Hewa Duniani (World Meteorological Day).

Siku hii ni muhimu kwa ajili ya kuadhimisha kuanzishwa kwa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) na kuangazia jukumu muhimu la huduma za kitaifa za hali ya hewa katika kuhakikisha usalama wa wananchi na mali zao.









**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Wilbert Muruke
Nasry Msulwa

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya



www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

TMAonline_TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.